# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 29 Aprili, 2020**

*(Bunge lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

(*Maswali yafuatayo Yameulizwa na Kujibiwa kwa kwa njia ya Mtandao)*

Na. 173

**Hitaji la Afya Kituo cha Afya Mtowisa**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Kituo cha Afya Mtowisa kina upungufu Mkubwa wa watumishi (Waganga) na hivyo kusababisha msongamano wa wagonjwa:-

Je, ni lini Serikali itapeleka waganga wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Mtowisa kina watumishi 29. Kwa mujibu wa Ikama ya Watumishi wa Afya ya Mwaka 2014 – 2019, Kituo cha Afya kinatakiwa kuwa na watumishi kuanzia 39 hadi 52. Hivyo kina upungufu wa watumishi 10 kukidhi ikama inayohitajika. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetangaza nafasi 610 za ajira za Watumishi wa Afya ambao wataajiriwa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo Halmashauri ya Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ili kutatua changamoto hiyo.

Na. 174

**Ujenzi wa Barabara Tarafa ya Ussoke - Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Wananchi wa Urambo wanaishukuru Serikali kupitia TARURA kwa kutengeneza barabara za Urambo Mjini ili ziweze kupitika na kuchochea maendeleo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara za Tarafa ya Ussoke kwa kuanzia na barabara inayopita katikati ya Mji wa Ussoke ili nayo iweze kupitika kwa kuwekewa lami na mifereji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TARURA* inaendelea na ujenzi wa mitaro ya maji yenye urefu wa kilomita moja kwa kiwango cha zege katika Tarafa ya Ussoke ili kulinda barabara zilizojengwa zisiharibike. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na uboreshaji wa barabara zenye urefu wa kilomita 14.5 zilizoko katika Mji wa Ussoke ili ziweze kupitika wakati wote.

Na. 175

**Kumalizia Ujenzi-Kituo cha Afya Chumo**

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE** aliuliza:-

Tarafa ya Kipatimu haina Kituo cha Afya cha Serikali na hivyo kusababisha wananchi katika Tarafa hii kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kupata huduma za matibabu:-

Je, Serikali iko tayari kusaidia juhudi za wananchi wa Kata ya Chumo kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya ulioanza kwa nguvu za wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedasto Edgar Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo iko tayari kukamilisha miundombinu ya kutolea huduma za afya iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi kikiwemo Kituo cha Afya Chumo. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imetenga Shilingi milioni 40 kuanza ujenzi.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, zimetengwa Shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kituo hicho.

Na.176

**Ahadi ya Mradi Mkubwa wa Maji – Jimbo la Mlimba**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Mwaka 2019 Waziri wa Maji alipokuja Mlimba aliwaahidi kuwa ifikapo mwezi Desemba, Serikali italeta fedha na Wahandisi ili kutekeleza mradi wa maji mkubwa ambao utasambazwa katika Kata za Chisano, Kalengakelo, Kamwene na Mlimba, lakini hadi Februari, 2020 mradi huo bado haujaanza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa maji Mlimba utafanyika katika awamu mbili. Mpango wa muda mfupi utahusisha kuboresha huduma ya maji katika vijiji vitano kati ya 10 vilivyopo kata za Mlimba, Kamwene na Kalengakelu. Kazi hiyo inatarajiwa kuchukua miezi sita kuanzia mwezi Aprili, 2020.

Mheshimiwa Spika, kisima cha maji cha Kijiji cha Matema chenye uwezo wa mita za ujazo 30 kwa saa kitaunganishwa kwenye tenki la mita za ujazo 45 lililopo Kamwene na tenki la mita za ujazo 400 lililopo Mlimba ili kuongeza huduma ya maji Vijiji vya Mlimba A, Mlimba B, Mwembeni na Kamwene. Tayari kiasi cha shilingi milioni 300 zimetolewa mwezi Februari, 2020 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mpango wa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu utahusisha ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Mto Udagaji umbali wa kilomita 28 hadi Mlimba. Mradi huu

utahudumia Kata za Mlimba, Chisano, Kalengakelu, Kamwene na Ching'anda zenye jumla ya vijii 10 ambavyo ni Mlimba A, Mlimba B, Mwembeni, Kamwene, Mlimba Msolwa, Chisano, Mgugwe, Ngwasi, Udagaji na Kalengakelu.

Na. 177

## Kigezo Kinachotumika Kupanga Bei ya Zao la Mahindi

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Wananchi wa Mkoa wa Rukwa hususan Jimbo la Nkasi Kusini ni wakulima wazuri wa zao la mahindi na gharama za uzalishaji wa zao hili kwa hekari inakadiriwa kufika shilingi 700,000/= ambapo mapato ni wastani wa gunia 15 hadi 17. Serikali kupitia Shirika lake la *NFRA* wametoa bei elekezi ya shilingi 380 kwa kilo, bei ambayo haiwezi kurudisha gharama za uzalishaji:-

Je, ni kigezo gani kinatumika kupanga bei ya zao hili?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Majukumu mahsusi ya *NFRA* ni kuhakikisha usalama wa chakula kwa kununua na kuhifadhi akiba ya chakula ili kukabiliana na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza nchini kutokana na majanga mbalimbali. Kiasi cha nafaka kinachonunuliwa kila msimu kinategemea na nafasi iliyo wazi ghalani, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kununua akiba ya Taifa ya Chakula pamoja na hali ya uzalishaji wa ziada ya chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, kulingana na uwezo wa sasa wa *NFRA* kuhifadhi kuwa tani 251,000 tu nchi nzima, *NFRA* hununua nafaka chini ya 2% ya ziada iliyozalishwa nchini. Hivyo ununuzi wa nafaka hutegemea zaidi sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, *NFRA* huingia sokoni kununua nafaka kama mnunuzi mwingine yeyote katika soko huru. *NFRA* kama taasisi nyingine au sekta binafsi, hukutana na ushindani wa bei katika ununuzi wa nafaka na hata pale inapofikia hatua ya kuzungusha akiba ya chakula katika masoko.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kununua akiba ya chakula, *NFRA* inatumia bei za kununulia mazao kwa kuzingatia bei za soko zinazozingatia ugavi na mahitaji ili kutokuharibu mfumo wa soko na kuzoofisha jitihada za sekta binafsi kushiriki katika biashara ya nafaka nchini.

Mheshimiwa Spika, bei iliyotumika katika ununuzi wa msimu wa mwaka 2018/2019 imezingatia bei za soko katika kununua mahindi. Bei hizo pia zilizingatia gharama nyingine ambazo mkulima anazipata katika uzalishaji. Hivyo kufanya bei zilizotumiwa na Wakala kuwa juu zaidi ya wanunuzi wengine wote katika masoko ya Tanzania kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano msimu huu Wakala umenunua mahindi kwa bei ya kati ya shilingi 350/= hadi shilingi 500/= kwa kilo kwa kulingana na hali ya soko katika maeneo husika ya ununuzi. Aidha, bei hizo ni juu ya wastani wa bei kwa maeneo husika ambapo bei za mahindi zimekuwa chini kufikia shilingi 200/= na hata shilingi 170/= kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, kigezo kinachotumika ni bei ya soko linalozingatia ugavi wa uzalishaji na mahitaji ya soko na mlaji wa mahindi kwa wakati husika na siyo gharama za uzalishaji. Kutokana na wakulima wengine kushindwa kulima kwa kutumia mbinu za kisasa za kilimo, siyo rahisi kwa *NFRA* kutumia bei ya kununulia nafaka ambayo itaweza kukidhi matakwa ya kila mkulima.

Aidha, wakati wa kutekeleza kazi ya ununuzi, *NFRA* hulipa ushuru wa mazao *(Produce Cess)* kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982.

Na. 178

**Malalamiko juu ya Uvuvi katika Ziwa Victoria**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto nyingi katika uvuvi wa Ziwa Victoria unaosababisha malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa uvuvi:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha inamaliza malalamiko haya?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndilla Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikishughulikia malalamiko, kero na matatizo ya wavuvi kwa kufanya vikao na mikutano na wavuvi pamoja na wadau wa uvuvi nchi nzima ili kuwasikiliza na kupata maelezo ya kina kuhusiana na malalamiko au matatizo yao. Aidha, Wizara imekuwa ikipokea malalamiko au kero na matatizo ya wavuvi na wadau wa uvuvi hususan wa Kanda ya Ziwa Victoria kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, malalamiko mengi ya wavuvi na wadau wa uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria yaliyokuwepo wakati wa Operesheni Sangara 2018 iliyolenga kupambana na uvuvi haramu. Wizara imeyashughulikia kikamilifu na kuyatatua. Malalamiko makubwa yaliyoshughulikiwa ni pamoja na ukomo wa kuvua sangara wenye urefu wa sentimeta 85 ambapo ukomo uliondolewa, matumizi ya taa za *solar* ambapo sasa zinaruhusiwa kwa kufanya marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepunguza tozo mbalimbali za usafirishaji wa samaki na mazao yake ikiwemo

kayabo, vichwa vya samaki na vifua. Vilevile, maboresho makubwa ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 ambayo yatajibu kwa upana changamoto za uvuvi, wavuvi na wadau wa uvuvi yanaendelea kufanyika ambapo yamewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Fedha kupata maoni yao kabla ya kukamilishwa.

Na. 179

**Kutambua Maeneo Mapya Yenye Vivutio vya Utalii**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Sekta ya Utalii ni moja kati ya vyanzo vikuu vya mapato kwa uchumi wa nchi yetu na Serikali ya Awamu ya Tano ina dhamira ya dhati kuinua sekta hiyo muhimu; na katika kufanya hivyo, Kilindi ni moja kati ya maeneo yenye vivutio vya utalii kama vile mlima mfano wa mama aliyembeba mwana, Pori Tengefu la Handeni, pamoja na maeneo yenye uoto wa asili katika Kata ya Lwanda katika Kijiji cha Lukigo.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuyatambua maeneo hayo rasmi ya utalii?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kuwa, Sekta ya Utalii ni moja kati ya vyanzo vikuu vya mapato kwa uchumi wa nchi, ambapo kwa mwaka 2019 sekta hii ilichangia takriban jumla ya Dola za Marekani bilioni 2.6 katika uchumi wa nchi. Aidha, sekta hii huchangia zaidi ya asilimia 25 ya mauzo yote ya nje na hutoa ajira zaidi ya milioni 1.5 kati ya ajira zote za moja kwa moja na zile ambazo siyo za moja kwa moja. Utalii ni sekta mtambuka, hivyo imeendelea kuwa chachu kwa maendeleo

ya sekta nyingine za uchumi kama vile kilimo, viwanda, huduma za fedha na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya jukumu la Wizara yangu ni kubaini, kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii nchini kwa kushirikiana na mamlaka za Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya.

Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara inaendelea kubaini vivutio vya utalii katika mikoa mbalimbali nchini kwa lengo la kuhamasisha uendelezaji wake na kuvitangaza ili maeneo hayo yaweze kutembelewa na watalii na hivyo kuongeza kipato kwa wananchi wanaozunguka maeneo hayo na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Tanga, kazi hiyo imeshafanyika kwenye Wilaya za Tanga Mjini, Muheza, Pangani na Mkinga. Kwa kuwa kazi hii ni endelevu, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri zote za Mkoa wa Tanga itaendelea kupitia vivutio vya utalii vilivyopo mkoani humo vikiwemo ambavyo vipo Wilayani Kilindi mfano Pori Tengefu la Handeni, kwa lengo la kuviendeleza na kuvitangaza.

Na. 180

**Kuwawezesha Wananchi wanaoishi karibu na Hifadhi za Misitu Biharamulo**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza: -

Asilimia 54 ya eneo la Wilaya ya Biharamulo ni Hifadhi ya Misitu na Mapori ya Akiba:-

Je, Serikali inafanya jitihada gani kuwawezesha wananchi wanaoishi katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi hizo kushiriki katika uchumi unaoendana na mazingira hayo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba eneo kubwa la Wilaya ya Biharamulo ni Hifadhi ya Misitu na Mapori ya Akiba. Kwa upande wa hifadhi ya misitu, Wilaya ya Biharamulo ina hifadhi mbili za misitu ambayo ni Msitu wa Hifadhi wa Biharamulo na Msitu wa Hifadhi wa Nyantakara. Msitu wa Hifadhi wa Biharamulo unazungukwa na vijiji 17 wakati msitu wa Nyantakara umezungukwa na vijiji 10.

Mheshimiwa Spika, kupitia sera yetu ya ujirani mwema, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)* ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa hifadhi hizo za misitu, umekuwa ukiwawezesha wananchi kufanya shughuli mbalimbali rafiki kwa mazingira ikiwemo ufugaji nyuki na upandaji miti. Jumla ya mizinga 3,848 imetundikwa ndani ya hifadhi hizo za misitu kwa wananchi wapatao 805 walio katika vikundi 30.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wakala umetoa mafunzo ya upandaji miti na kuwezesha kuotesha miche ya miti kwa wanufaika 76 kutoka Shule ya Msingi Nemba, Kikundi cha Ujasiriamali Biharamulo *(BiDiG)* na Magereza-Biharamulo. Pia, kwa mwaka 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilipata mgao wa jumla ya shilingi 8,248,257/= kutokana na mapato ya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Spika, vilevile, jumla ya miche 60,000 imeandaliwa ambayo inatarajiwa kugawiwa kwa wananchi hao tayari kwa kupandwa katika msimu huu wa mvua. Aidha, wananchi 115 wanaofanya biashara za mazao ya misitu walipatiwa mafunzo ya namna bora ya kufanya biashara hiyo kwa kuzingatia taratibu na kanuni zilizopo ili kukuza uchumi wa viwanda kupitia mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, kutundika mizinga tu haitoshi kupata mazao mengi ya nyuki na yenye ubora. Wakala pia, umetoa mafunzo kwa wananchi 185 walio katika maeneo

ya Biharamulo Mjini, Lusahunga, Nyakanazi, Kaniha, Nemba na Nyantakara kuhusu namna bora ya kufungasha mazao ya nyuki na hivyo kuongeza wigo wa soko na kukuza kipato.

Mheshimiwa Spika, mafunzo pia yalitolewa kuhusu umuhimu wa kutumia mizinga ya kisasa ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki. Kwa ujumla Wakala utaendelea na mikakati mbalimbali ili kuwezesha wananchi hao kuendelea kufaidika na rasilimali za misitu zilizopo.

Na. 181

**Elimu bila malipo kwa Shule za Umma**

**MHE. SUZAN P. MASSELE** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa sababu gani Serikali imeshindwa kutekeleza kikamilifu na kwa ufanisi mkakati wa utoaji elimu bila malipo katika Shule za Umma?

(b) Je, ni kwa nini shule nyingi za Serikali za Umma zinakabiliwa na mazingira magumu ya kufundishia na kujifunzia ikilinganishwa na zile za binafsi? Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto hizo?

(c) Je, ni kwa nini Shule za Serikali huwa haziathiriwi na ukaguzi unaofanywa na Idara ya Ukaguzi wa Elimu kama inavyokuwa kwa shule za binafsi?

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Peter Massele, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa Elimumsingi bila Malipo, Serikali hutoa kiasi cha shilingi bilioni 23.8 kila mwezi kwa ajili ya kugharamia Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, posho za madaraka kwa Wakuu wa Shule na Maafisa Elimu Kata na fidia za ada ya Mitihani ya Kidato cha

Nne. Tangu kuanza kwa mpango huo kumekuwa na mafanikio makubwa katika uandikishaji na mahudhurio ya wanafunzi shuleni. Kwa mfano, mwaka 2014 jumla ya wanafunzi 1,464,376 waliandikishwa Darasa la Kwanza ikilinganishwa na wanafunzi 1,810,814 walioandikishwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya shule na kuandaa vitabu vya kiada ili kukabiliana na changamoto ya ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mwaka 2019/2020 Serikali imechapa na kusambaza vitabu vya kiada 1,359,350 vya Elimu ya Awali hadi Darasa la V kwa uwiano wa 1:3. Aidha, nakala za vitabu vya kiada 1,567,537 za masomo ya Kiswahili, Sayansi, Hisabati na Sanaa zimesambazwa katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika kipindi cha mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020 Serikali imekarabati shule kongwe 73 na kukamilisha maboma 2,815. Katika kuhakikisha elimu inatolewa katika ubora unaotakiwa, Serikali imeendelea kuimarisha idara ya Uthibiti Ubora wa shule kwa kuongeza Wathibiti Ubora wa shule wapya 400 pamoja na kujenga Ofisi za Uthibiti Ubora wa shule katika Halmashauri 100 nchini.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule ni kufanya tathmini katika shule zote za Serikali na zisizo za Serikali kwa lengo la kuhakikisha kwamba shule hizo zinatoa elimu bora kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo. Endapo kuna ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utoaji elimu katika shule husika, Idara humshauri mmiliki wa shule ya Serikali au isiyo ya Serikali ili kufanya maboresho. Ikiwa mmiliki atashindwa kufanya maboresho, Idara humshauri Kamishna wa Elimu ili kuchukua hatua stahiki bila kujali ni Shule ya Serikali au isiyo ya Serikali.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI -KATIBU MEZANI**

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko makubwa ninaomba kuwajulisha kuwa Bunge letu limepatwa na msiba mwingine mkubwa wa kuondokewa na mwenzetu, Mbunge wa Jimbo la Sumve kupitia Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, ambaye amefariki usiku wa kuamkia leo tarehe 29 Aprili, 2020 hapa Jijini Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia msiba huo uliotupata, taratibu mbalimbali za mazishi zimeanza kufanyika kwa mawasiliano kati ya Ofisi yetu ya Bunge pamoja na familia ya Marehemu na upande wa Serikali na kila tukipata taarifa zaidi za kuwataarifu, tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Marehemu Ndassa mmoja wa Wabunge ambao tulikuwa tukiwaita ni *senators* alikuwa ni miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge waandamizi, walioingia humu Bungeni toka mwaka 1995. Amekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve kwa vipindi vitano mfululizo. Hii inaonesha imani kubwa waliyokuwa nayo Wananchi wa Sumve, ambaye walimwamini sana na Wabunge wengi tunaweza tukajifunza uongozi bora kwa kufuata nyayo zake.

Hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 152 ya Kanuni ya Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Kwa siku ya leo hatutaendelea na Kikao cha Bunge, badala yake tutakuwa na maombolezo ya msiba wa mwenzetu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa tusimame kwa muda kama ishara ya kuomboleza kifo cha mwenzetu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kuomboleza kifo cha Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa - Mbunge wa Sumve)*

**SPIKA:** Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi, Amina.

Naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokuambieni, tumepata msiba huu mkubwa alfajiri ya leo. Tutajitahidi sana kwa kadiri iwezekanavyo kuhakikisha kwamba Mheshimiwa huyu ndugu yetu, anazikwa kule Sumve kesho jioni. Tutajitahidi sana *unless strongly* tumekuwa *advised otherwise*. Kwa sababu kwa mila zetu za kiafrika, kwa kweli kumzika mtu popote pale ni jambo linalotupa ugumu sana.

Fikiria yeyote uliyepo hapa upatwe na jambo kama hilo halafu unawekwa popote! Ni ngumu sana. Kwa hiyo, tutajitahidi sana. Kwa hiyo, Ofisi yangu itashirikiana na Serikali kuona kila kinachowezekana kinafanyika ili Mwenyezi Mungu akiwa upande wetu basi hilo liweze kutekelezwa.

Nawaomba Tume ya Huduma za Bunge tukutane hapa kwenye Ukumbi wa Spika mara tu baada ya kuahirisha Kikao hiki ili tuweze kuzingatia hili lililojitokeza kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa sasa kama nilivyowaeleza shughuli za leo haziwezi kuendelea mpaka kesho, naomba sasa niahirishe Shughuli za Bunge hadi kesho saa 8.00 mchana.

*(Saa 8.08 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 30 Aprili, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*